# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

# FAHARI YA SAME

***Maendeleo Daima***

***Toleo la Machi 2023 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***

## MADIWANI SAME WAPITISHA BAJETI YA TSH.BIL 60.9



***Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba akizungumza katika kikao maalum cha Baraza la  Bajeti, kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Halmashauri Mhe Yusto Mapande na kulia ni Mhe Mkuu wa Wilaya Kasilda Mgeni .***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepitisha Bajeti ya Shilingi bilioni 60.9 kwa mwaka wa fedha 2023/24 ikijumuisha fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo,mishahara ya Watumishi na matumizi ya Ofisi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Anastazia Tutuba amesema bajeti hiyo ina ongezeko la asilimia 5.62 ya bajeti ya mwaka 2022/23 ambayo ilikuwa bilioni 60.4.

Tutuba amevitaja vipaumbele katika bajeti hiyo kuwa ni pamoja na kumalizia miradi viporo ambayo mingi ni ya Afya na Elimu ikijumuisha umaliziaji wa zahanati nne na umaliziaji wa madarasa kwa shule za Msingi na Sekondari.

“Kama Halmashauri tuna vipaumbele muhimu katika utekelezaji wa bajeti hii ikiwemo ujenzi wa jengo la kitega uchumi PADECO kwani tutakapokamilisha jengo hili litasaidia kuongeza mapato ya Halmashauri”alisema Mkurugenzi.

Ameyataja maeneo mengine ya vipaumbele katika bajeti hiyo kuwa ni pamoja na kujenga Ofisi za vijiji,kutoa mikopo isiyo na riba kwa wanawake ,vijana na watu wenye ulemavu ili kuwainua kiuchumi,kujenga mifereji ya umwagiliaji na kujenga nyumba za Walimu.

Aidha Mkurugenzi huyo amesema kwa mwaka wa fedha 2023/24 Wilaya hiyo inalenga kukusanya mapato ya ndani shilingi bilioni 3.4 kutoka bilioni 2.9 za mwaka wa fedha unaoishia Juni 30,2023.

Amesema ili kufikia lengo la ukusanyaji huyo Halmashauri imeimarisha mifumo yake ya kukusanya mapato pamoja na kujiwekea lengo la ununuzi wa Mashine za kukusanyia mapato (POS) 15 ili kuhakikisha kuwa kila eneo lenye mapato lina mashine na wakala wa kukusanya mapato.

Halmashauri ya Wilaya ya Same inategemea mapato yake kutokana na ushuru wa madini ya ujenzi,ushuru wa mazao mbalimbali,faini zinazotokana na makosa mbalimbali.



***Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakifuatilia uwasilishaji wa makisio ya Bajeti.***

## KASILDA MGENI-MKUU MPYA WA WILAYA YA SAME.



***Mkuu wa Wilaya ya Same.Mhe Kasilda Mgeni akila kiapo cha utii katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.***

Wilaya ya Same imepata Mkuu wa Wilaya mpya Mhe:Kasilda Jeremiah Mgeni kufuatia uteuzi na mabadiliko ya vituo vya kazi kwa Wakuu wa Wilaya yaliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe:Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa mwezi Februari 2023.

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Same Edward Mpogolo ambaye amehamishiwa Wilaya ya Ilala alikabidhi ofisi kwa Mkuu mpya wa Wilaya ya Same Mhe: Mgeni ambapo alimwambia kazi kubwa iliyopo mbele yake ni usimamizi wa miradi ya Maendeleo na usimamizi wa makusanyo ya mapato ya Halmashauri.

Mpogolo amesema Wilaya ya Same inatekeleza Miradi mbalimbali ambayo inahitaji ufuatiliaji wa karibu wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ili iweze kukamilika katika ubora unaotarajiwa.

"Wilaya ya Same inatekeleza miradi mingi ikiwemo Ujenzi wa Hospitali mpya ya Wilaya,Ujenzi wa Vituo vya Afya,Shule mpya za Sekondari mbili,soko la barabarani la Kirinjiko,Jengo la wagonjwa wa dharura katika hospitali ya Wilaya,hii ni baadhi tu ya Miradi inayohitaji usimamizi"alisema Mpogolo.

Kwa upande wa ukusanyaji wa mapato,Mkuu huyo wa Wilaya aliyeondoka alimjulisha Mhe:Mgeni kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wilaya imelenga kukusanya shilingi bilioni 2.9 na tayari zimeshakusanywa bilioni 1.9.

Aidha Mpogolo alimpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Anastazia Tutuba kwa usimamizi mzuri wa Miradi na ushirikiano mzuri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kwa kipindi chote ambacho Mkuu huyo wa Wilaya amekuwepo Same.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa Ofisi Mkuu huyo wa Wilaya aliahidi kuendeleza yale yote yaliyokuwa yanasimamiwa na mtangulizi wake katika Ofisi hiyo ili kuhakikisha kuwa Mipango na Malengo ya Serikali yanatimia.

“Nimshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kunileta Wilaya ya Same na nimuahidi ndugu yangu Mpogolo kwamba nitaendelea pale alipoishia yeye na tutaendelea kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha Wilaya inakuwa imara kiuchumi na Miradi yote nitaifuatilia kwa karibu” alisema Mhe:Mgeni.




Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe. Edward Mpogolo (kushoto) ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Wilaya ya Ilala akimuaga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu ofisini kwake.

**TAMISEMI YAIPATIA SAME PIKIPIKI ZA WATENDAJI KATA**



***Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe Kasilda Mgeni Akikabidhi Pikipiki zilizotolewa na Tamisemi kwa Watendaji wa Kata Wilayani humo.***

Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe Kasilda Mgeni amekabidhi pikipiki sita zilizotolewa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa watendaji wa Kata Wilayani Same ili kuboresha shughuli za utendaji.

Akikabidhi pikipiki hizo Mkuu huyo wa Wilaya amewataka watendaji kutumia pikipiki hiyo kwa malengo tarajiwa ya kuboresha utoaji wa huduma na ukusanyaji wa mapato ya serikali.

"Serikali imewathamini na kuwapatia Vitendea kazi,hivyo ni vyema pikipiki hizo zikatunzwa na kutumika kwa malengo tarajiwa"alisema Mhe:Mgeni
Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Anastazia Tutuba ameishukuru Ofisi ya Rais Tamisemi kwa Msaada huo ambao amesema utasaidia kuboresha utendaji kazi.

Naishukuru Sana Ofisi ya Rais Tamisemi kwa kutupatia pikipiki hizi ambazo tuna imani kubwa kuwa zitasaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato.

"Kwa mwaka 2021 Halmashauri yetu ilifanikiwa kununua pikipiki 16 za watendaji wa Kata,hivyo tayari Kata 22 kati ya 34 zina pikipiki,lengo ni kuhakikisha kata zote zinapata pikipiki"alisema Tutuba

Nae Mtendaji Kata wa Mshewa, Benedict Lopa ameishukuru serikali kwa kuwapatia Vitendea kazi na kuahidi kutumia kwa malengo tarajiwa.

## HALMASHAURI YATAIFISHA MBAO ZENYE THAMANI YA MIL 7.3



***Baadhi ya Mbao zilizotaifishwa na serikali kutoka kata ya Vunta baada ya mmiliki wake kukosa vibali halali vya uvunaji wa mbao hizo.***

Katika kudhibiti upotevu wa mapato,halmashauri ya Wilaya ya Same imetaifisha vipande 1,765 vya mbao vyenye thamani ya shilingi milioni 7.3 baada ya kupatikana zikiwa zimevunwa bila kibali katika Kata ya Vunta Wilayani humo.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo Anastazia Tutuba amesema kuwa ni kosa kisheria kuvuna miti na kupasua mbao bila kufuata utaratibu ambao ni kujadiliwa katika Kijiji husika na kupewa Muhtasari wa kukubaliwa ukiambatana na barua ya Mtendaji Kijiji ndipo uweze kupatiwa kibali.

Tutuba amesema kuwa mnamo Novemba 17,2022 ofisi yake ilipata taarifa kuwa kuna mbao zimevunwa katika Vijiji vya Papa,Vunta na Kidunda katika Kata ya Vunta ambapo alituma timu kufuatilia ambapo mbao hizo zilipatikana.

Anasema baada ya mbao hizo kupatikana Mtendaji Kata aliagizwa kuzilinda na kutangaza katika vijiji vyote kama kuna mtu anayehusika na mbao hizo afike Halmashauri kwaajili ya kuzilipia na kulipa faini kwa kuvuna miti na kupasua mbao bila kibali.

“Sheria inatutaka kukaa siku 30 yaani mwezi mmoja kusubiri mwenye mbao hizo kujitokeza ili alipe faini lakini mwezi mmoja ulipita akiwa hajajitokeza ndipo Halmashauri ilipotangaza kutaifisha mbao hizi na mapato yake yataingia serikalini”alisema Tutuba.

Kwa Upande wake Kaimu Afisa Misitu wa Wilaya ya Same,Ally Mangwaya alisema Ofisi yake inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha kwamba Sheria ya Misitu inafuatwa ili kulinda Misitu.

“Kuvuna na kumiliki mali ya misitu bila kuwa na vibali vya uvunaji ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na.14ya mwaka 2002 sura namba 323 vifungu vya 85 na 88 na Sheria hiyo katika kifungu cha 94(4) inaelekeza iwapo mhusika atashindwa kujitokeza kulipa faini ndani ya siku 30 basi Mali hizo zinatakiwa kutaisfishwa na Serikali”alifafanua Mangwaya.

Alisema Sheria hiyo ndiyo imeipa Halmashauri mamlaka ya kutaifisha mbao hizo ili iwe fundisho kwa wengine wasiofuata utaratibu wa uvunaji wa mazao ya Misitu.

## DC SAME AWAAGIZA RUWASA KUCHIMBA VISIMA KWA WINGI

Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe  Kasilda Mgeni ameitaka Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilayani humo kuendelea kuchimba visima vya maji ili kusaidia upatikanaji wa maji wa uhakikika kwa wakazi wa Same Mjini,Makanya na Hedaru.

Mhe Mgeni alitoa wito huo wakati wa maadhimisho ya wiki ya maji yaliyofanyika kiwilaya katika Kijiji cha Gundusine kwenye Kata ya Hedaru ambapo alisema RUWASA bado wana kazi kubwa ya kufanyaili  kuhakikisha kuwa wananchi wa Same katika maeneo ya mjini wanapata maji ya uhakika.

“Wote tunajua kwamba Serikali  imetupatia zaidi ya shilingi bilioni sita kwaajili ya Mradi mkubwa wa maji wa Same -Mwanga -Korogwe mbao utakapokamilika utamaliza kabisa shida ya maji katika miji yetu ya Same,Mwanga na Korogwe lakini wakati tunasubiri Mradi huu kukamilika RUWASA chimbeni Visima kukabiliana na changamoto ya maji kwa wakati huu”amesema Mkuu huyo wa Wilaya.

Mkuu huyo wa Wilaya  amesema serikali imetoa gari ya kuchimba visima virefu kwa kila mkoa ukiwemo Mkoa wa Kilimanjaro hivyo gari hilo litumike kuchimba visima na kumaliza kero ya maji katika maeneo yote ya Same.

Maadhimisho kya wiki ya maji katika Wilaya ya Same yalijumuisha kupanda miti katika chanzo cha maji cha Gundusine ili kutunza mazingira katika chanzo hicho ambacho kinategemewa kuhudumia wananchi wote wa Hedaru.

Aidha Mkuu wa Wilaya alitoa onyo kwa wananchi wote wanaolima ndani ya mita 60 kutoka katika vyanzo vyote vya maji ikiwemo chanzo cha maji cha Gundusine ambapo aliwataka kuacha mara moja kwani kufanya hivyo ni kuharibu chanzo cha maji.

Nimeona mmeotesha mahindi jirani kabisa na chanzo cha maji,hii sio sawa,mnaharibu chanzo cha maji na maji yatakauka hivyo naagiza yale mahindi yakishavunwa msilime tena, na atakayekaidi sheria itachukua mkondo wake"alisema Mhe Mgeni.

Awali akitoa taarifa ya maji katika Wilaya hiyo,Kaimu Meneja wa RUWASA Wilaya ya Same Mhandisi John Kasmir  alisema tayari wamefanikiwa kufikisha huduma kwa wananchi wa vijijini zaidi ya asilimia 80.

Alisema kwa upande wa Mjini wameweza kuchimba visima vinne ambavyo  vinasaidia kutoa huduma kwa wananchi huku Mradi mkubwa wa Same-Mwanga –Korogwe ukiwa katika hatua ya kulaza mabomba.

Alisema tayari mabomba makubwa yameshalazwa katika kilomita 17 na ya kusambazia maji mjini yamelazwa kilomita 20 huku kazi hiyo na Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi  May mwaka kesho.

Maadhimisho ya wiki ya maji kwa mwaka 2023 yameongozwa na kaulimbiu isemayo"KUONGEZA KASI YA MABADILIKO KATIKA SEKTA YA MAJI KWA MAENDELEO ENDELEVU YA UCHUMI"

## SAME YAPATA ZAIDI YA TANI 400 ZA MAHINDI YA GHARAMA NAFUU



***Mahindi ya gharama nafuu toka Wakala wa Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA)yakishushuwa Wilayani Same.***

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepokea zaidi ya Tani 468.25 za Mahindi ya gharama nafuu kutoka Wakala wa Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA) Ofisi ya Arusha ili kusaidia wananchi wenye uhitaji kutokana na uhaba wa chakula Wilayni hapa.

Kwa miaka miwili mfululizo Wilaya ya Same imekosa mvua za kuaminika kwa misimu ya masika na vuli hivyo kuhatarisha uhakika wa chakula kwa kaya mbalimbali.

Afisa Kilimo wa Wilaya Omar Mhina amesema tayari tani 386.6 zimeshauzwa kwa wananchi mbalimbali wenye uhitaji na bado Wilaya inaendelea kupokea maombi ya wenye uhitaji ili waweze kunufaika na mahindi hayo.

“Utaratibu wa kupata mahindi haya unaanzi kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ambaye ataorodhesha majina ya wananchi wenye uhitaji na kuyawasilisha kwa msimamizi wa mahindi hayo toka NRFA ambapo atapatiwa namba ya malipo na wakishalipia ndipo watakapopatiwa mahindi kama Kijiji au Mtaa na kuyagawa kwa wananchi wao”alifafanua Mhina.

Mhina amesema kuwa kila mtu amekadiriwa kutumia kg 50 kwa mwezi  na anaruhusiwa kuchukua mahindi ya kumtosha kwa miezi mitatu,kama ana familia tunahesabu kila kichwa kg 50 kwa mwezi na haruhusiwi kuchukua chakula kinachozidi miezi mitatu  ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na mahindi hayo.

Kwa upande wake Afisa wa Kilimo anayesimamia kituo cha Same,Debora Mtati amesema mahindi hayo ambayo yamefungashwa katika mifuko ya kilo 50 kila mmoja huuzwa kwa shilingi 885 kwa kilo moja ambapo mfuko mzima ni shilingi 44,250.

Afisa huyo anasema kuwa ili kuepuka upotevu wa mahindi hawapimi kwa kilo mojamoja badala yake wanashauri wananchi ambao hawawezi kununua mfuko wa kilo 50 waungane kwa makundi katika vijiji vyao ili waweze kumudu kulipia mfuko mmoja.

## MWENYEKITI AWAAGIZA WAKANDARASI WA BARABARA KULIPA USHURU WA VIFUSI

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Mhe: Yusto Mapande amewataka wakandarasi wanaojenga barabara Wilayani humo kuhakikisha wanalipia ushuri wa vifusi ambao ni shilingi elfu tano kwa kila kifusi.

Akizungumza katika Baraza la madiwani mwezi Februari Mwenyekiti huyo alimwagiza Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini (TARURA) Wilayani humo,Mhandisi Baraka Libungo kuhakikisha kuwa wakandarasi wanalipia vifusi vyote wanavyotumia katika ukarabati wa barabara.

Mapande alisema kumekuwa na tabia ya wakandarasi wanaofika kukarabati barabara za vijijini kutojitambusha katika ofisi za serikali lakini pia kufanya kazi na kuondoka bila kulipia vifusi ambavyo wanachimba katika maeneo ya vijiji.

“Hawa wakandarasi ni wafanyabiashara na wanapokuja kwenye maeneo yetu wanachimba vifusi bure lakini tunachotaka sisi sio malipo ya hivi vifusi bali ni ushuru tuu wa serikali wa shilingi elfu tano tu lakini bado hawataki kulipa wanatukwepa”alisema Mwenyekiti huyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Anastazia Tutuba amesema halmashauri hiyo inadai zaidi ya milioni 5 ushuru wa vifusi toka kwa wakandarasi mbalimbali wanaotengeneza barabara wilayani humo.

“Fedha hizi zinakusanywa na Watendaji Kata na Mawakala wetu wa mapato lakini hawa watu hawalipi,niseme tu kwamba sasa sheria itachukua mkondo wake maana tunapoteza mapato”amesema Tutuba.

Kwa Upande wake Mhandisi Libungo aliahidi kufuatilia wakandarasi hao na kuwaagiza kulipa fedha hizo ili kuchangia mapato ya serikali”kama kuna wakandarasi wanadaiwa ushuru wa vifusi tunaomba majina ya kampuni zao au tujulishwe ni wa barabara ipi ili kama hawalipi kwa hiari tuwakate kwenye malipo yao”alisema Libungo

## SERIKALI KUWATAFUTIA WANAWAKE WAASIRIAMALI MASOKO




***Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe Kasilda Mgeni akizungumza na Wanawake katika maadhimisho ya kilele cha siku ya Wanawake Duniani, yaliyofanyika kimkoa Wilayani Same,pembeni yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri Anastazia Tutuba***

Serikali mkoani Kilimanjaro imeahidi kuwatafutia wajasiriamali wanawake masoko ya bidhaa mbalimbali wanazozalisha ili waweze kujikimu kiuchumi.

Ahadi hiyo imetolewa leo na Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe:Kasilda Mgeni ambaye amemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa  Kilimanjaro Mhe:Nurdin Babu katika sherehe za kilele cha siku ya wanawake Duniani zilizofanyika kimkoa Wilayani Same.

Mhe:Mgeni alitoa ahadi hiyo baada ya kutembelea mabanda ya maonyesho ya bidhaa mbalimbali za wajasiriamali wanawake.

Baada ya kutembelea mabanda ya maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali wamenieleza kuwa changamoto yao kubwa ni masoko ya uhakika hivyo naahidi kuwa Serikali itajitahidi kutafuta masoko ya bidhaa hizi ndani na nje ya nchi"alisema Mhe:Mgeni.

Awali akitembelea banda la mjasiriamali wa viungo mbalimbali vya chakula,Halima Kilusu na mjasiriamali Catherine Wales anayetengeneza batiki wote walilalamikia kukosa masoko ya uhakika ya bidhaa zao.

Wales amemuomba Mkuu wa Mkoa kuwasaidia katika kupata masoko ya uhakika ya bidhaa wanazozalisha.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Anastazia Tutuba alisema Ofisi yake itaendelea kuwawezesha wanawake wajasiriamali kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba.

"Tutaendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia mikopo isiyo na riba ya Halmashauri,wajiunge katika vikundi vya watu wasiopungua watano,wasajili vikundi vyao,waje kuomba mikopo"alisema Tutuba

Tutuba amesema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri hiyo inatarajia kutoa mikopo isiyo na riba ya Wanawake,Vijana na Walemavu yenye thamani ya shilingi milioni 700

## WANAWAKE WILAYANI SAME WATOA MSAAADA KWA WATOTO WENYE MAHITAJI MAALUM



*Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe Kasilda Mgeni (aliyesimama katikati) akiwa katika picha ya pamoja na wanawake na wanaume waliowasindikiza kukabidhi misaada kwa watoto wenye mahitaji maalum wilayani humo kama sehemu ya madhimisho ya siku ya wanawake duniani.*

Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe Kasilda Mgeni kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anastazia Tutuba pamoja na wanawake wengine Wilayani humo

wamefanikiwa kutoa misaada mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalum kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani.

Timu hiyo ya wanawake Wilayani Same imefanikiwa kutembelea na kutoa misaada mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalum wa shule za Msingi Same na Kisima,Kituo cha kulea watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi cha RAFIKI na Mama Mlemavu Mwanaisha Hamisi ambaye ana watoto wawili walemavu.

Akiongoza timu hiyo,Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe:Kasilda Mgeni alisema misaada hiyo imetolea kama sehemu ya maadhimisho ya wiki ya wanawake ambayo kilele chake ni Machi 8 ya kila mwaka.

Akiwa katika Shule ya Msingi Kisima Mkuu wa Wilaya aliwapongeza waalimu kwa kuweza kuwasimamia na kuwalea vema watoto hao wenye usonji ambao wanahitaji uangalizi wa karibu.

Kwa namna ya kipekee kabisa niwapongeze walimu kwani naelewa kulea watoto hawa kuna changamoto nyingi lakini mmesimama imara kuhakikisha kuwa wanapata elimu iliyo bora"alisema Mkuu huyo.

Nae Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Anastazia Tutuba amewapongeza wanawake wa Same kwa kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii katika kuelekea siku ya wanawake duniani Machi 8.

"Ni michango ya wanawake ndio imetuwezesha kuwatembelea watoto na watu wengine wenye uhitaji,wanawake tuendelee kushikamana"alisema Tutuba.

Kwa upande wake Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo Jasmini Haji aliwashukuru wanawake Wilayani Same kwa msaada waliowapatia.

"Tunashukuru kwa msaada huu na tunaomba Mwenyezi Mungu awaongezee pale walipopunguza"alisema Mwl.Haji

**MSD YAGAWA VYANDARUA 85,272 KWA WANAFUNZI WILAYANI SAME**




***Katibu Tawala wa Wilaya ya Same,Sospeter Magonera akikata utepe kuzindua zoezi la ugawaji vyandarua kwa Wanafunzi Wilayani Same,Magonera alimwakilisha Mkuu wa Wilaya Mhe Kasilda Mgeni,pamoja nae ni Mkurugenzi wa Halmashauri,Anastazia Tutuba na mwakilishi wa Mganga wa Wilaya TAudesia Kilawe.***

Bohari kuu ya dawa (msd) Kanda ya Kilimanjaro imeanza zoezi la kugawa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za Msingi katika Wilaya ya Same ili kupunguza maambukizi ya Ugonjwa wa Malaria.

Wakigawa vyandarua kwa Wanafunzi wa shule ya Msingi Same, Kaimu Meneja wa msd Kanda ya Kilimanjaro Florida Sianga alisema katika Wilaya ya Same wanatarajia kugawa vyandarua 85,272/-kwa shule 209 za Msingi za serikali na binafsi.

"Lengo la Serikali ni kutokomeza kabisa ugonjwa hatari wa malaria kwahiyo kwa kugawa vyandarua hivi na vikitumika vizuri tuna hakika maambikizi ya malaria yatapungua"amesema Meneja huyo.

Akizungumza wakati wa kugawa vyandarua hivyo Katibu Tawala wa Wilaya ya Same (DAS),Sospeter Magonera ambaye alimwakilisha Mkuu Wilaya hiyo Mhe:Kasilda Mgeni ameonya baadhi ya watumishi wasio waaminifu ambao huuza vyandarua hivyo vya bure.

"Natoa onyo kwa walimu ambao shule zao zimepewa vyandarua kuhakikisha kuwa vyandarua hivi vinawafikia walengwa ambao ni wanafunzi,ole wake atakayejaribu kuuza vyandarua hivi vya bure"alionya DAS huyo.

Nae Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Anastazia Tutuba ameonya vyandarua hivyo visitumike kulimia mbogamboga.

Tutuba alisema Serikali Wilayani humo itawachukulia hatua wale wote watakaotumia vyandarua hivyo kwa matumizi tofauti na yanayotarajiwa.

Mwanafunzi Naomi Msuya wa Shule ya Msingi Same,amemshukuru Mhe:Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapatia vyandarua vya bure ili kuwalinda na Malaria.

Akizungumzia hali ya maambukizi ya Malaria Wilayani Same,Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Same Taudesia Kilawe alisema kwa Mkoa wa Kilimanjaro Wilaya ya Same inaongoza kwa kuwa na maambukizi ya juu ya Malaria ambapo kwa wagonjwa wa nje (OPD) waliotibiwa mwaka 2020 asilimia 1.6 walikutwa na maambukizi ya Malaria na kwa mwaka 2021 ilishuka kufikia asilimia 1 ambapo 2022 ilifika asilimia 0.5.

## WWF YAFADHILI UTAFITI WA SIMBA HIFADHI YA MKOMAZI



***Simba na watoto wake akiwa katika moja ya hifadhi nchini Tanzania***

Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF) limefadhili Mradi endelevu kwaajili ya kufanya utafiti wa Simba katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi iliyopo Wilayani Same.

Akitambulisha Mradi huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe Kasilda Mgeni,Mkurugenzi Mkazi wa WWF Profesa Noah Sitati alisema utafiti utajumuisha kujua idadi ya Simba waliopo Mkomazi lakini pia Simba watafungwa Camera maalum za ufuatiliaji.

Mradi huu wa miaka mitatu utatekelezwa katika Wilaya za Longido,Mwanga na Same na lengo lake ni kutambua masuala mbalimbali kuhusu Simba ambapo watayatolea taarifa ili Serikali na wadau wengine wa wanyama waweze kuchukua hatua'amesema Profesa Sitati.

Msimamizi wa Mradi huo Emanuel Kivuyo amesema kwa sasa Mkomazi inakadiriwa kuwa na Simba 34 tu hivyo utafiti utakapokamilika utaweza kubainisha kama Simba hao wanapungua na ni nini sababu ya kupungua kwao ili kuweza kuishauri serikali nini kifanyike.

Kivuyo anasema Mradi huo unatarajia kuanza utekelezaji mwezi Julai mwaka huu,anasema ni kawaida kwa wanyama kupungua na kuongezeka kwahiyo tafiti zitasaidia serikali na wadau wengine wa Wanyamapori kujipanga kulingana na matokeo ya utafiti.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe Kasilda Mgeni aliupokea Mradi huo na kuahidi kutoa ushirikiano utakaowezesha kufanikiwa kwa Mradi huo kwa kadri utakavyohitajika.

"Niwakaribishe sana Wilaya ya Same,tunashkuru kwa kuichagua Wilaya yetu kama sehemu ya kufanya utafiti huu na tutawapa ushirikiano wa kutosha"Alisema Mhe Mgeni.

## WALIOOMBA UMEME SAME KUUNGANISHIWA JULAI 2023

Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) Wilaya ya Same limeahidi kuwaunganishia umeme wananchi walioomba kuunganishiwa huduma hiyo hasa maeneo ya mjini ambayo bado hayajapata umeme mwezi Julai 2023.

Kaimu Meneja wa TANESCO wilaya ya Same Mhandisi Fabian Ruhumbika amesema hayo wakati akijibu swali la Thea Emil mkazi wa Same aliyetaka kufahamu ni lini wananchi walioomba umme watapatiwa huduma hiyo.

Emil aliuliza swali hilo katika Mkutano wa kusikiliza kero za Wananchi ulioandaliwa na na Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe:Kasilda Mgeni uliofanyika katika viwanja vya stendi kuu ya mabasi wilayani Same.

Mwananchi huyo alitaka kufahamu kwanini wamewasilisha maombi ya kuunganishiwa huduma ya umeme lakini bado hawajapatiwa huduma hiyo.

Katika majibu yake Meneja huyo alisemawaombaji wapya watapatiwa umeme katika bajeti ya mwaka 23/24 itakayoanza utekelezaji wake mwezi Julai 2023baada ya kupatiwa fedha za utekelezaji wa miradi ya shirika hilo ikiwemo kuunganisha umeme.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Same,Mhe:Kasilda Mgeni ameitaka TANESCO wilayani humo kuhakikisha kuwa waombaji wote wa umeme wanapatiwa umeme ili kupunguza malalamiko kwa wananchi.

“Mheshimiwa Rais anataka wananchi wote wapatiwe huduma ya umeme na amekuwa kileta fedha kwaajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya TANESCO hivyo tusimwangushe Rais tuhakikishe kuwa wananchi wanaumgamishiwa umeme” amesema Mhe: Kasilda,




**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138,SAME**

***Mhariri wa Mkuu:Anastazia Tutuba***

***Mhariri wa Habari:Amina Sangawe***

***sMachi 2023 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***